TANGAZO LA SERIKALI NA 527 la tarehe 21/9/2018

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA 290

_____

SHERIA NDOGO

_____

(Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))

_____

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA ZA MWAKA, 2018

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Newala za mwaka, 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya Newala.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:-

"Ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali, na leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa masuuli" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri au afisa yeyote atakayeidhinishwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia

utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Bidhaa"maana yake ni kitu chochote chenye thamani kilicholetwa sokoni au gulioni kwa lengo la kuuzwa.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Newala;

"Kibali' maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri

"Leseni" maana yake ni kibali cha maandishi kinachotolewa kwa mtu binafsi, kampuni au taasisi kinachoruhusu kufanya biashara au shughuli yoyote katika eneo la Halmashauri.

"Machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala pamoja na Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mkataba" maana yake ni makubaliano yenye nguvu ya sheria ya ununuzi au uuzaji au utoaji wa huduma yo yote kati ya Halmashauri na mdau husika.

"Ushuru''maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala kwa ajili ya huduma mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni Mtu, Taasisi, Kampuni au asasi yoyote iliyoteuliwa kwa mujibu wa Sheria na Halmashauri kukusanya mapato

kwa niaba ya Halmashauri.

Ada naUshuru

4. (1) Halmashauri itatoza Ada naUshuru katika biashara, huduma, vibali, au leseni mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoorodheshwa kwenye jedwali la kwanza Sheria Ndogo hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla kifungu kidogo cha (1) cha 4 cha Sheria Ndogo hizi Halmashauri itatoza Ada na Ushuru katika vyanzo vifuatavyo:-kama ambavyo imeanishwa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi

i. ushuru wa Mazao;
ii. ushuru wa ukaguzi wa nyama;
iii. uda ya kununua zabuni za Halmashauri;
iv. ushuru wa samaki;
v. ushuru wa madini ya ujenzi;
vi. ada ya kukodisha mali za Halmashauri;
vii. ada ya Machinjio;
viii. ada ya kuendesha shughuli za Utamaduni; burudani na michezo;
ix. ada yaUpimaji wa ardhi na vibali vya ujenzi;
x. ada ya zabuni;
xi. ada ya kununua vitabu vya zabuni;
xii. ushuru wa maegesho ya magari;
xiii. ushuru wa stendi;
xiv. ushuru ya minada;

Namna ya kukusanya Ada naUshuru

5 (1) Halmashauri itaweka utaratibu kadri itakavyoona inafaa ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo maalum ya kutoza Ada na Ushuru kutoka vyanzo vya mapato kama ilivyoainishwa kwenye kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo hizi.

(2) Malipo ya Ada au Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au wakala na kutolewa stakabadhi halali ya kielektroniki kama kielelezo cha malipo

yaliofanyika.

(3) (a) Ada unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kupata huduma, leseni au kibali husika.

(b)ushuru utozwao na Halmashauri utalipwa wakati wa kupata huduma au baada ya kupata huduma

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 5 cha Sheria Ndogo hizi Halmashauri au wakala kwa idhini ya Afisa Masuuli itatoa kwa mlipaji stakabadhi halali ya kawaida kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika endapo stakabadhi ya kielektroniki haiwezi kutolewa.

(5) Halmashauri au Wakala atakuwa na mamlaka ya kukamata bidhaa au mali ya mtu yeyote endapo ameshindwa kulipa Ushuru ndani ya muda aliotakiwa kulipa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(6) Endapo bidhaa au mali iliyokamatwa na Halmashauri au wakala haitalipiwa Ushuru unaodaiwa ndani ya siku 7 kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka, na ndani ya siku 2 kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka kwa kibali cha mahakama. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuuza bidhaa au mali na fedha zitakazopatika na zitawekwa kwenye akaunti ya Halmashauri.

(7) Wakala hataruhusiwa kuuza au kufanya jambo lolote kwa mali au bidhaa iliyokamatwa bila kupata idhini ya Afisa Masuuli.

Wajibu wa kulipa Ada

6 (1) Ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada au Ushuru kulipa kiwango hicho kama ilivyoainishwa

auUshuru

kwenye Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni wajibu kwa kila mtu kutoa taarifa sahihi kwa Halmashauri au Wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.

(3) Itakuwa ni wajibu kwa kila mtu atakayelipa Ada au Ushuru kutunza kumbukumbu za malipo.

Kibali au leseni

7. (1) Halmashauri itatoa kibali au leseni kwa mfanyabiashara au mtu yeyote kwa kadri itakavyoona inafaa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni wajibu kwa kila mfanyabiashara au mtu yeyote anayetaka kufanya jambo lolote linalohitaji kibali au leseni kuomba na kupata leseni au kibali kutoka Halmashauri.

Uteuzi wa wakala

8. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua Kampuni au Taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria, kukusanya Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa wakala

9. Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa:-

(a) Kukusanya Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alililopangiwa na kwa kiwango kilichoidhinishwa katika ya Sheria Ndogo hizi;

(b) Wakala atakusanya Ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Makosa kwa Wakala

10. Itakuwa ni kosa kwa Wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo:-

(1) atashindwa, atadharau, atakwepa au atakataa kulipa Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa

na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada au Ushuru.

(3) atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi

(4) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ushuru ndani ya Halmashauri

(5) atashindwa au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ushuru

(6) atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya Ushuru.

Uwezo wa Afisa mwidhiniwa

11. 1) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote au jengo lolote kwa nia ya kukusanya au kufanya tathimini au kufanya jambo lolote linalohusiana na Ada, Ushuru, leseni au Kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa

12. Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mtu yeyote:-

1) atashindwa, atadharau, atakwepa au atakataa kulipa Ada au Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.
2) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada au Ushuru.
3) atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria

Ndogo hizi.

4) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada au Ushuru ndani ya Halmashauri.
5) atashindwa kutoa taarifa sahihi au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.
6) atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya Ada au Ushuru.

Kufifilisha Makosa

13. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria hizi, kiasi kisichozidi shilingi laki tano (Tsh. 500, 000/=) na kisichopungua shilingi laki mbili (200,000)iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi, na atatakiwa kulipa Ada na Ushuru aliokwepa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

14. Mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa, na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua laki mbili (200,000) na isiyozidi shilingi milioni moja (Tsh.1000, 000/=) au kifungu kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au vyote kwa pamoja.

Tangazo na. 314/2014

15 Sheria Ndogo hii inafuta Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Newala za Mwaka 2014.

JEDWALI LA KWANZA

Limetungwa chini ya kifungu cha 4(2)

SEHEMU YA KWANZA

Ushuru wa Mazao

Na	Aina ya chanzo	Kiasi cha Ushuru
1.	Korosho	Asilimia 5% ya bei ya kuuza
2.	Ufuta	Asilimia 5% ya bei ya kuuza
3.	Mpunga	Asilimia 5% ya bei ya kuuza
4.	Muhogo	Asilimia 5% ya bei ya kuuza
5.	Mahindi	Asilimia 5% ya bei ya kuuza
6.	Viazi	Asilimia 5% ya bei ya kuuza
7.	Vitunguu	Asilimia 5% ya bei ya kuuza
8.	Karoti	Asilimia 5% ya bei ya kuuza
9.	Ndizi	Asilimia 5% ya bei ya kuuza
10	Mboga	Asilimia 5% ya bei ya kuuza
11	Matunda	Asilimia 5% ya
12	Mbaazi	bei ya kuuza
13	Kunde	Asilimia 5% ya
14	Karanga	bei yakuuza
15	Njugu	Asilimia 5% ya bei ya kuuza
		Asilimia 5% ya bei ya kuuza

		Asilimia 5% ya bei yakuuza
16.	Mazao mengineyo	Asilimia 5% ya bei ya kuuza

SEHEMU YA PILI

Ada ya kununua zabuni za Halmashauri	Tshs.100,000/= kwa kila kitabu cha zabuni.

SEHEMU YA TATU

Ada ya zabuni	Asilimia moja (1%) ya malipo kwa kila hati malipo.

SEHEMU YA NNE

Ushuru wa samaki

1.	Kamba	Tshs.300 kwa kilogramu moja
2.	Kambale	Tshs.300 kwa kilogramu moja
3.	Dagaa	Tshs.300 kwa kilogramu moja

SEHEMU YA TANO

Ushuru wa madini ya ujenzi.

1.	Fomu ya maombi ya kibali cha kuchimba madini ya ujenzi	Tsh 3000/= kwa kila fomu
2	Kibali cha kuchimba madini ya ujenzi	Tshs 150,000/= kwa kila kibali
3.	Madini ya ujenzi tani 1 hadi 3	Tshs.3000/= kwa kila safari
3.	Madini ya ujenzi tani 4 hadi 7	Tshs.5000/= kwa kila safari Tshs1000/= kwa kila tani itakayoongezeka

SEHEMU YA SITA

Ada ya kukodisha mali za Halmashauri;

1.	Kukodi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya Mikutano/vikao na sherehe	Kwa mujibu wa Mkataba
2.	Kukodi uwanja wa Halmashauri	Kwa mujibu wa Mkataba
3.	Vibanda vya biashara	Kwa mujibu wa Mkataba

SEHEMU YA SABA

Ada ya Machinjio, Ukaguzi wa nyama na Ushuru wa Bucha

1.	Ushuru, ukaguzi na machinjio ya nyama kwa kila ng'ombe atakayechinjwa.	Tshs. 5000/=
2.	Ada ya ukaguzi na machinjio wa nyama kwa kila kondoo, Mbuzi na nguruwe atakayechinjwa.	Tshs.2500/=

3	Ushuru wa ngozi ya ngo'mbe	Tshs 500/=
4.	Ushuru wa ngozi ya mbuzi	Tshs 300/=
5.	Kuku/ Bata kwa Tenga	Tshs 1000/=

SEHEMU YA NANE

Ada ya kuendesha shughuli za Utamaduni, burudani na michezo;

1.	Kibali cha ngoma za jadi	Tshs.50,000/= kwa kila kibali
2.	Kibali cha kuchezesha disco, Maonyesho ya bendi, Sanaa za maonyesho, mazingaumbwe, sinema, video, matamasha na Matamasha	Tshs.30,000 kwa onyesho,
3.	Kibali cha kuchezesha michezo ya kubahatisha	Tshs. 30,000/= kwa kila mchezo
4.	Kibali cha Mechi za Mipira katika viwanja vya taasisi za Halmashauri	Tshs.50,000/= kwa kila ligi
5.	Ada ya Mganga wa Jadi aliyesajiliwa	Tshs 50,000/= kwa mwaka
6	Kibali cha promosheni za bidhaa	Tshs 50,000/= kwa kila kibali
7	Ada ya pool table	Tshs 50,000/= kwa kila mwezi

SEHEMU YA TISA

Ada ya Upimaji wa ardhi na vibali vya ujenzi.

1.	Ada ya Fomu ya ya maombi ya ardhi	Tshs 20,000/=
2.	Kibali cha ujenzi	
	(a) Jengo la makazi	15,000/= kwa kibali
	(b)Jengo la makazi gorofa moja	50,000/= kwa kibali

(c)Jengo la makazi zaidi ya gorofa moja	100,000/= kwa kibali
(d)Jengo la makazi na biashara	150,000/= kwa kibali
(e)Jengo la biashara	200,000/= kwa kibali
(f)Jengo la biashara zaidi ya gorofa 1	250,000/= kwa kibali
(g)Jengo la kiwanda	500,000/= Kwa kibali
(h)Jengo la taasisi	500,000/= Kwa kibali

SEHEMU YA KUMI
USHURU WA MAEGESHO

Na	AINA YA CHOMBO CHA USAFIRI	KIASI CHA USHURU KWA SIKU
1.	Pikipiki iliyosajiliwa kwa Biashara katika maeneo yaliyotengwa	500/=
2.	Teksi	500/=
3.	Lori chini ya tani 7/Pick up/Basi dogo	5 00/=
4.	Lori zaidi ya Tani 7/Basi kubwa	1,000/=
5.	Magari mengine yasiyo ya biashara	500/=

USHURU WA MAENEO YA MAEGESHO MAALUM

Na	Aina ya chombo cha usafiri	Kiasi cha ushuru kwa siku
1.	Teksi	3000/=

2.	Lori chini ya tani 7/Pick up/Basi dogo	5000/=
3.	Lori zaidi ya Tani 7/Basi kubwa	5000/=
4.	Magari mengine yasiyo ya biashara	3000/=

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

USHURU WA STENDI

.

Ushuru wa kuingiza stendi vyombo vya usafiri	*Kiwango cha ushuru(Tshs)kwa siku*
a) Pikipiki	300/=
b) Teksi/ Gari ndogo chini ya abiria 5	500/=
c) Basi chini ya abiria 25 (Hiace)	1,000/=
d) Basi kubwa la abiria (Coaster)	2,000/=
e) Basi zaidi ya abiria	2,500/=

MAGARI YANAYOTOKA NJE YA WILAYA

(a) Ushuru wa gari ndogo ya biashara …… ……1,500/=
(b) Ushuru wa gari binafsi …… ……1,000/=
(c) Ushuru wa gari kubwa ……..2,000/=
(d) Ushuru wa mkokoteni kwa siku moja ……300/=

ADA YA KULAZA MAGARI YALIYOTOKA SAFARINI (ON TRANSIT) KWA SIKU MOJA

(a) Magari Madogo ya watu binafsi
……..……..2,500/=
(b) Magari Makubwa ya binafsi (lori au basi)
…….4,000/=
(c) Mashine na mitambo ya ujenzi wa barabara
……5,000/=

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

Ada ya minada ya soko Bidhaa yoyote itakayouzwa kwa jumla katika mnada.	Itatozwa Asilimia 10% ya bei ya mauzo kwa kila bidhaa.

JEDWALI YA PILI
Limetungwa chini ya kifungu cha 13

KUFIFILISHA KOSA

Mimi …….…….……wa S.L.P…….…….. nakiri kwa hiari yangu mbele ya……..ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Newala kwamba mnamo tarehe……ya Mwezi….Mwaka……nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha 13 cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya Newala za mwaka 2018.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Newala. Niko tayari kulipa kiasi cha Ada na Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIYARI YANGU KWA KADIRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……..ya mwezi……mwaka……
Jina……..…….…….……...Saini……...

Mbele ya:

Jina……..……

Saini…….….

Wadhifa…….……

Nembo ya Halmashauri imegongwa katika Sheria Ndogo hizo kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Newala uliofanyika mnamo Tarehe 24 Mwezi wa 04 Mwaka 2017 na Nembo iliyogongwa mbele ya:-

MUSSA M. CHIMAE
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya
Newala

L.S

RASHID CHITWANGA. NDEMBO,
Mwenyekiti,
Halmashauri ya Wilaya ya
Newala

NAKUBALI,

Dodoma,
27Agost 2018

SELEMANI S.JAFO (MB)
Waziri wa Nchi-or Tamisemi